TAARIFA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO MHESHIMIWA DKT. SHUKURU JUMANNE KAWAMBWA (MB) KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA UFUNGUZI WA MKUTANO WA WADAU WA SEKTA YA MIFUGO DODOMA, TAREHE 03 OKTOBA 2006

Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Edward N. Lowassa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Mkutano

Mheshimiwa William Lukuvi (Mb), Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi

Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mali Asili na Mazingira

Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya

Waheshimiwa Wabunge

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Dodoma

Makatibu Wakuu na Makatibu Tawala wa Mikoa

Waheshimiwa Wahisani wa Nchi mbalimbali

Wawakilishi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali

Ndugu Wafugaji

Ndugu Wageni waalikwa

Mabibi na Mabwana

Mheshimiwa Rais,

Awali ya yote napenda kuwakaribisha rasmi kwenye mkutano huu wa wadau wa Sekta ya Mifugo nchini. Aidha, napenda kutoa shukurani zetu za dhati kwako kwa kukubali mwaliko wetu wa kutufungulia mkutano huu. Pamoja na shughuli nyingi za kitaifa zinazokukabili umeweza kutenga muda kuja kuongea na wadau wa Sekta hii. Mhe Rais, tunatambua pia kuwa ulikuwa kwenye safari nje ya nchi ukikabiliwa na shughuli nyingi na inawezekana ukawa umechoka, lakini bado umeona umuhimu wa kuja kutufungulia mkutano huu. Tunakushukuru sana kwa kutupatia heshima hii kubwa.

Mheshimiwa Rais,

Napenda pia kumshukuru sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa (Mb) kwa kukubali kuitisha na kuwa mwenyekiti wa Mkutano huu wa Wadau wa Sekta ya Mifugo. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametimiza ahadi yake aliyoitoa bungeni wakati akiahirisha Mkutano wa Nne wa Bunge la Bajeti hapa Dodoma tarehe 16/8/2006.Tunampongeza sana.

Mheshimiwa Rais,

Mkutano huu wa Wadau wa Sekta ya Mifugo unafuatia Mkutano uliyofanyika Arusha mwaka 2001 na kufunguliwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Mkutano huo ulianisha matatizo yanayofanya ufugaji wetu usiweze kutoa mchango unaostahili kwa pato la Taifa na kuwaondolea wafugaji umaskini. Aidha, mkutano huo uliweka Dira ya Sekta ya Mifugo ambayo inatekeleza Dira ya Taifa ya mwaka 2025 na Malengo ya

Kitaifa ya Millenia (Millenium Development Goals - MDGs). Mheshimiwa Rais Mstaafu wakati akihutubia mkutano huo alitoa changamoto zifuatazo kwa wadau.

1. ***Maisha ya Wafugaji****: Ni kwa nini mifugo ambayo ni mali, haijaweza kuboresha maisha ya wafugaji walio wengi?*
2. ***Mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye uchumi*** *: Kwa nini mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye uchumi wa maeneo ya wafugaji na hatimaye kwenye uchumi wa taifa, bado ni mdogo?*
3. ***Ufugaji kibiashara na viwanda:*** *Ni kwa nini ufugaji wa kisasa, wa kibiashara pamoja na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo bado umedumaa?*

Vilevile, Mheshimiwa Rais Mstaafu alitoa rai ambayo napenda kunukuu

"***Natoa rai tufanye mambo ya uhakika, ubabaishaji uwe mwiko. Sera za jumla za uchumi sasa ziko tayari kuhimili ukuaji wa uchumi ikiwemo sekta ndogo ya mifugo. Wakati wa kubadili gia ya maendeleo ya ufugaji na taifa letu ni sasa. Tusiogope kufanya maamuzi. Tusiogope kuthubutu. Tusiogope kubadili maisha na mienendo tuliyoizoea. Nina hakika tukishirikiana na kusaidiana tutafanikiwa.***"

Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Rais,

Katika kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania uliunda Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ili kusimamia kwa

ufanisi zaidi maendeleo ya wafugaji nchini. Kuanzishwa kwa Wizara hii kumeleta changamoto kubwa kwa wadau wa Sekta.

Mheshimiwa Rais

Wizara inatekeleza kwa makini maagizo uliyoyatoa wakati wa uzinduzi wa Bunge pamoja na yale uliyoyatoa wakati ulipotembelea Wizara yetu. Kwetu sisi maagizo hayo na maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005 na mwelekeo wa Sera za CCM katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2010 ni changamoto na fursa ya kusukuma ukuaji na uendelezaji wa mifugo, chini ya falsafa yako ya "Ari mpya, Nguvu mpya na Kasi mpya". Hii inatokana na ukweli kwamba Sekta ya Mifugo ina umuhimu mkubwa katika kuchangia kukuza uchumi wa taifa letu na kumwondolea mfugaji umaskini kwani zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi vijijini kwa kutegemea kilimo, ufugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Rais

Naomba sasa uniruhusu nitoe kwa kifupi taarifa kuhusu baadhi ya maeneo ya Sekta ya Mifugo:

(i) Rasilimali ya Mifugo

Nchi yetu ina rasilimali kubwa ya mifugo. Tunao takribani ng'ombe milioni 18.5, mbuzi milioni 13.1, kondoo milioni 3.5, kuku milioni 50, na nguruwe milioni 1.2. Aidha, takribani asilimia 97 ya mifugo yetu ni ya asili yenye ukosaafu mdogo (*low genetic potential*) hivyo kuwa na viwango vidogo vya uzalishaji pamoja na kwamba ina uwezo mkubwa wa kustahimili magonjwa na kuhimili mazingira

magumu. Ufugaji wa mfumo wa asili umegawanywa kwenye makundi mawli unaojumuisha wafugaji wa kuhamahama (*pastoralists*) na wafugaji-wakulima (*agro-pastoralists*) na takribani asilimia 3 tu ndiyo ipo chini ya mfumo wa kibiashara.

(ii) Uchimbaji malambo

Mheshimiwa Rais,

Ukosefu wa maji ni chanzo kimojawapo cha wafugaji kuhamahama na hatimaye kusababisha migongano kati yao na watumiaji wengine. Ili kuipatia mifugo yetu maji, Wizara imechangia uchimbaji/ukarabati wa malambo **278** katika wilaya **48** ambapo malambo **150** yamekamilika. Uchimbaji/ukarabati wa malambo haya umefanyika kwa ushirikiano kati ya Serikali, wananchi na Halmashauri za Wilaya. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Wizara itachangia ujenzi wa malambo 20 na mabwawa mawili. Vilevile, kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs), malambo 35 yatachimbwa. Tayari tumetuma fedha za kuchimba malambo katika Wilaya za Nachingwea, Lindi, Kilwa na Chunya ili kujiandaa kupokea mifugo kutoka Ihefu, na vilevile tumetuma fedha nyingine Kishapu na Mwanga ili kupunguza athari ya ukame.

(iii) Ukarabati na Ujenzi wa Majosho Mapya

Mheshimiwa Rais,

Tunayo majosho **2,050** na kati ya hayo ni majosho **808** tu yanayofanya kazi. Kutokana na majosho mengi kuharibika, kuanzia mwaka 2002/2003, Serikali ilichukua hatua za makusudi za kuanza kuyakarabati baada ya Halmashauri za

Wilaya kushindwa kuyaendesha. Serikali kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (**DADPs**) ilitoa **shilingi bilioni 1.6** kwa ajili ya kukarabati majosho **335** na sekta binafsi ilikarabati jumla ya majosho **47.** Baada ya ukarabati huo, hukabidhiwa kwa Halmashauri za Wilaya ili vikundi vya wafugaji viweze kuyaendesha. Napenda kukiri kwamba ingawaje ufufuaji wa majosho unaenda taratibu lakini wafugaji wanaonyesha nia thabiti ya kuogesha. Naamini mchango wa Serikali kupitia ruzuku itakayotolewa mwaka huu ya shilingi bilioni 2 itasaidia sana kufufua uogeshaji. Bila shaka mifugo mingi itaokoka kutokana na magonjwa yaletwayo na kupe.

(iv) Uzalishaji na Usambazaji wa Teknologia za Mifugo

Mheshimiwa Rais,

Katika jitihada za kuzalisha na kusambaza ng'ombe na mbuzi wa maziwa kwa wafugaji nchini, hususan wenye kipato kidogo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kusambaza ng'ombe na mbuzi bora wa maziwa kwa wafugaji wadogo chini ya utaratibu uliobuniwa wa "*kopa ng'ombe/mbuzi lipa ng'ombe/mbuzi*". Ng'ombe bora wa maziwa waliongezeka na kufikia **434,760** mwaka 2005 kutoka **212,334** mwaka 1995. Mwaka 2005/2006 mitamba wa maziwa **5,120** walizambazwa kwa wafugaji. Vilevile, mbuzi wa maziwa waliongezeka kutoka **13,500** mwaka 1995 na kufikia mbuzi **75,761** mwaka 2005. Katika mwaka 2005/2006 jumla ya mbuzi wa maziwa **1,196** walizambazwa kwa wafugaji.

Pamoja na ongezeko hilo la ng'ombe wa maziwa na nyama, nia ya Wizara yangu ni kuboresha mifugo ya asili kwa kuchanganya na mbegu bora. Ng'ombe aina ya Mpwapwa ambao wamefikia 1,000 kwa sasa wanatarajiwa kuzalishwa kwa wingi kama mbadala wa ng'ombe wa asili. Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa itaendelea kuimarishwa ili kuendeleza teknolijia mpya na sahihi zitakazoongeza uzito na uzalishaji wa ng'ombe hao.

Eneo jingine lililoonyesha mafanikio japo kwa kiwango kidogo ni uzalishaji wa mazao ya mifugo ambapo uzalishaji wa maziwa uliongezeka hadi kufikia lita **bilioni 1.41** mwaka 2005/2006 na uzalishaji wa nyama ulifikia tani **388,294** mwaka 2005/2006. Kwa wastani ongezeko hili ni takribani asilimia 10 kwa mazao yote.

Ili kuendeleza uzalishaji na usimamizi wa mazao hayo Sheria ya Maziwa ilipitishwa mwaka 2004 na imeanza kutumika, hali kadhalika Sheria ya Nyama iko katika hatua za mwisho kupitishwa.

(v) Biashara ya Mifugo

Mheshimiwa Rais,

Nchi yetu imewekeana mikataba ya kibiashara yenye nafuu na nchi za ACP/EU chini ya mpango wa Economic Partnership Agreement (EPA) na inayo nafasi ya kufanya biashara na nchi za Afrika chini ya NEPAD na Marekani chini ya AGOA. Kwa nchi jirani tumeanza kufanya hivyo kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya nchi za SADC. Hivyo nchi yetu inayo nafasi kubwa ya kufanya biashara ya mifugo na mazao yake katika nchi hizo na tumeanza

kuitumia nafasi hiyo. Katika mwaka 2005/2006 nchi yetu imeuza nchini Comoro ng'ombe **1,706** na mbuzi **800** wenye thamani ya **shilingi milioni 675.9** na kufanya jumla ya ng'ombe **6,506** na mbuzi **2,790** wenye thamani ya Tshs **bilioni 2.056** kuuzwa nje tangu mwaka 2001/2002. Ili kuhakikisha kwamba mifugo na mazao yake yanakubalika katika masoko ya nje, Wizara imeanzisha Idara itakayoshughulikia utambuzi, ufuatiliaji na uandikishaji mifugo hai.

Vilevile, tumeanza kusafirisha nyama kwenda nchi za Ghuba ambapo tumeanza kuuza nyama ya mbuzi na kondoo katika nchi za Falme za Kiarabu na Kuwait. Mahitaji ya nchi hizo ni makubwa na kwa wakati huu wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani wanahitaji mbuzi 6,000 na kondoo 500. Tunajitahidi kutimiza kutimiza mahitaji hayo. Napenda kuwashukuru wafugaji wa mikoa ya Dodoma na Singida kwa kulichangamkia soko hili na kuitumia vyema machinjio ya Dodoma.

Mheshimiwa Rais,

Wizara imekamilisha ukarabati wa minada 52 ya mifugo, vituo vidogo 65 vya kupumzikia mifugo, vituo vikubwa 10 vya kupumzikia mifugo, vituo 11 vya kukagulia afya ya mifugo, vituo 7 vya kupakilia mifugo kwenye mabehewa pamoja na kukarabati mabehewa 50 ya kubebea mifugo. Aidha, jumla ya minada 7 ya mipakani imejengwa kwa lengo la kuimarisha biashara ya mifugo na nchi jirani. Pia, tangu mwaka 2003/2004, Wizara imeanza kutekeleza mpango wake wa kuendeleza miundombinu ya masoko kusini mwa Reli ya Kati ili kupanua biashara ya mifugo na nchi za SADC zilizo jirani na Tanzania.

Mheshimiwa Rais,

Katika miongo miwili iliyopita kumekuwepo na mabadiliko ya sera za uchumi za kijumla na kisekta zenye lengo la kuboresha huduma mbalimbali na kuvutia wawekezaji binafsi. Sekta ya Mifugo ni mojawapo iliyokumbwa na mabadiliko hayo. Tangu mwaka 1994 serikali ilijitoa katika kununua na kusambaza madawa ya mifugo nchini na kuachia sekta binafsi. Hata hivyo, sekta hii bado ni changa na inakabiliwa na matatizo mengi yakiwemo ya uhaba wa mitaji.

Hata hivyo, Wizara imebuni mikakati ya kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Mifugo ***(Strategic Investment Promotion in Livestock Sector)*** kama njia ya kutatua tatizo la uwekezaji katika Sekta. Hali hii ilitokana na uwekezaji mdogo ambapo kati ya mwaka 1990 na 2001, kati ya wawekezaji 1,844 ni 37 tu waliwekeza katika Sekta ya Mifugo, idadi ambayo ni sawa na asilimia 2 tu ya wawekezaji wote nchini. Sehemu kubwa ya uwekezaji katika Sekta ya Mifugo ni kwenye viwanda vya kusindika maziwa, nyama na ngozi na kidogo sana katika uzalishaji. Napenda kuwapongeza sana wawekezaji wachache kwa niaba ya wenzao ambao wameonyesha njia kwa dhati ikiwa ni pamoja na Sumbawanga Agricultural and Animal Feeds Industries Limited – SAAFI, Pride Meat wa Morogoro, Tanga Fresh, ASAS (Iringa), Tan Dairies (Dar es Salaam) na Mkuza Chicks Limited (Pwani).

(vi) Magonjwa ya Mifugo

Mwaka 2002 Serikali ilitoa **Waraka Namba 1** kuhusu Hatua za Kuzuia Kuenea kwa Magonjwa ya Mifugo Nchini. Waraka huo ni muhimu katika kuendeleza

sekta hii kwani magonjwa ni kikwazo kikubwa katika kufanya biashara ya mifugo na mazao yake na nchi nyingine. Pamoja na Waraka huo Sheria mbili za mifugo zilizopitishwa na Bunge mwezi Novemba, 2003 ikiwa ni pamoja na Sheria ya Kuzuia Magonjwa ya Mifugo (***Animal Disease Act 2003***) na Sheria ya Huduma za Mifugo (***Veterinary Act 2003***). Kupitishwa kwa sheria hizi kutasaidia kudhibiti magonjwa na kuboresha utoaji huduma za afya ya mifugo nchini, na mafanikio yake yameanza kuonekana.

Mheshimiwa Rais,

Kwa upande wa kinga dhidi ya magonjwa muhimu, chanjo dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu na Kichaa cha Mbwa zimeendelea kupewa kipaumbele na Serikali. Toka kuanzishwa kwa kampeni rasmi dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu mwaka 2000 dozi **milioni 26** zimenunuliwa kwa gharama ya shilingi **bilioni 2.** Kutokana na juhudi hizo za Serikali, matukio ya ugonjwa huu yanaendelea kupungua. Tafiti zinaonyesha ugonjwa huo umepungua kwa asilimia 50. Aidha, dozi **175,000** za chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa zimenunuliwa na kusambazwa katika wilaya **68** zilizokuwa na matukio mengi ya ugonjwa huo. Mkakati umeandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa nchini katika kipindi cha miaka mitano ijayo**.** Napenda kuwashukuru wenzetu hao kwa ushirikiano wao mkubwa. Vilevile ni matumaini yangu kwamba uimarishaji wa Maabara Kuu ya Mifugo ya Temeke uliofanyika hivi karibuni na ambao unaendelea utachangia kwa kiasi kikubwa kutambua kwa haraka magonjwa mbalimbali hapa nchini.

Mheshmiwa Rais,

Nchi yetu kama zilivyo nchi nyingi za Afrika, inakabiliwa na tishio la Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege (*Avian flu*). Kwa bahati nzuri hadi sasa hapajaripotiwa tukio lolote la ugonjwa huo hapa nchini. Serikali inaendelea kuchukua tahadhari ya kutosha. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Maliasili na Utalii zimeandaa Mpango wa Tahadhari kuhusu ugonjwa huo ambao unasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Ofisi hii inaendelea kuwasiliana na wahisani mbalimbali ili kupata fedha za kujihami.

Kuhusu kinga ya magonjwa ya kuku, kumekuwepo na mafanikio makubwa katika kudhibiti ugonjwa wa mdondo kwa kuku wa kienyeji vijijini kwa kutumia chanjo ambayo haihitaji kuhifadhiwa kwenye jokofu. Kwa mwaka jana pekee, jumla ya kuku **milioni 6.2** walichanjwa katika maeneo mbalimbali nchini na tathmini iliyofanyika inaonyesha kwamba vifo vya kuku vimepungua toka asilimia **90** hadi **5** pale ambapo chanjo imefanyika. Mafanikio haya ni ya kujivunia na hasa kwa kuzingatia kwamba kuku ni ndege anayeweza kufugwa na hata mwanakijiji au familia maskini, na hivyo kutoa nafasi ya kuwaondolea umaskini.

(vii) Zao la Ngozi

Mheshimiwa Rais,

Ngozi ni zao jingine lililoliingizia Taifa fedha za kigeni na kuongeza kipato cha wafugaji. Ngozi zilizouzwa nje baada ya kukaguliwa mwaka 2005/2006 ni

vipande milioni **1.6** vya ng'ombe, vipande milioni **1.4** vya mbuzi na vipande **950,000** vya kondoo vyenye thamani ya Tshs **bilioni 8.5.** Ubora wa ngozi unaonekana kuongezeka kutokana na juhudi za Serikali na msaada wa dola za Kimarekani **400,000** kutoka mfuko wa "***Common Fund for Commodities***" wa Shirika la FAO kwa ajili ya kuboresha zao hilo katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2004. Vilevile, Serikali imeanzisha Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo kutokana na ushuru wa asilimia 20 ya ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Juni, 2006 Shilingi **bilioni 5.0** zimekusanywa.

(viii) Mafunzo

Mheshimiwa Rais,

Wizara inaendesha mafunzo ya mifugo kwa wataalam wa kati katika Vyuo vyake vya Mpwapwa, Morogoro, Tengeru, Buhuri, Madaba na Temeke. Wataalam wa aina hii ndio wanaotoa huduma za kila siku kwa wafugaji.Kutokana na uboreshaji wa vyuo hivyo uliofanyika hivi karibuni, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi **154** hadi kufikia **770** mwaka 2005/2006 na idadi hii inaendelea kuongezeka kutokana na wanafunzi wengi kuanza kujigharamia. Vilevile, kwa kuvitumia vyuo hivi jumla ya wafugaji **1, 637** walipatiwa mafunzo.

(ix) Uwezeshaji wa Wananchi Kufuga Kisasa

Mheshimiwa Rais,

Utaratibu wa kuwawezesha wananchi kuingia kwenye ufugaji wa kati na mkubwa wa kibiashara umeendelea. Upimaji wa mashamba yaliyokuwa ya

Serikali na kuyagawa katika ranchi ndogo za hekta **4,000** ili wananchi waweze kuyaendeleza umefanyika katika mashamba ya Ranchi za Taifa (NARCO) ambapo mashamba **125** yalipatikana na kumilikishwa kwa wawekezaji binafsi na vikundi. Eneo hili lina ukbwa wa **ha 378,780** na uwezo wa kuweka ng'ombe **120,000**. Napenda kutoa taarifa kwamba jumla ya wawekezaji 21 tayari wameanza kuwekeza na Wizara yangu inaendelea kuwahamasisha wale ambao hawajaanza kuwekeza.

Mheshimiwa Rais,

Ili kuleta mapinduzi katika Sekta ya Mifugo ni sharti pawe na ushirikiano wa karibu kati ya wadau wote wa Sekta ya Mifugo. Wizara au Wafugaji peke yao hawawezi kufanikiwa katika kuinua kiwango cha ufugaji nchini. Lakini kwa pamoja, tukishirikiana kikamilifu, tukiwa na malengo yanayofanana, tutaweza kuleta mapinduzi katika ufugaji wetu katika miaka michache ijayo. Hivyo nachukua nafasi hii kuwashukuru wahisani na Asasi mbalimbali zinazojishughulisha na Sekta hii hapa nchini. Sisi sote, kwa kutekeleza yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ya mwaka 2005 kwa pamoja tutafanikiwa katika kufikia mapinduzi ya kweli ya ufugaji nchini.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wote walioshiriki kuandaa na kufanikisha Mkutano huu na hasa watoa mada watakaotoa changamoto mbalimbali kwetu. Aidha, nawashukuru wadau wote mliokubali mwaliko wetu kuhudhuria mkutano huu licha ya shughuli nyingi mlizonazo.

Mheshimiwa Rais,

Mwisho, naomba tena nichukue tena nafasi hii ya pekee ya kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa mgeni rasmi katika mkutano huu wa wadau wa sekta wa mifugo pamoja na kuwa na majukumu makubwa ya kitaifa yanayokukabili. Baada ya kusema hayo sasa, nafurahi kumkaribisha Mheshimiwa Waziri Mkuu ili akuombe utufungulie mkutano wetu.

Ahsanteni sana kwa Kunisikiliza